ELCT | EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA

Evangelical Lutheran Church in Tanzania (ELCT)
Boma Rd, Plot #66, P O Box 3033, Arusha, Tanzania
Website: www. elct.or.tz | Email: elcthq@elct.or.tz
Tel: +255 27 250 8856/7 | Fax: +255 27 254 8858 | SG. Direct line: +255 27 250 2511

# NENO LA KKKT KUHUSU MATUKIO YA WIKI YA UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA OKTOBA 2025

Ndugu wapendwa ninawasalimu katika Kristo Yesu.

Nchi yetu imefanya uchaguzi Mkuu wa Taifa tarehe 29 Oktoba 2025. Sote tunakumbuka kuwa siku hiyo na siku zilizofuata, nchi yetu imepitia hali ngumu ambayo haijawahi kutokea katika historia yake. Palitokea vurugu zilizosababisha upotevu wa maisha, ulemavu na uharibifu wa mali za umma na binafsi. Hakuna sababu yoyote inayotosheleza kueleza upotevu maisha na uharibifu wa mali. Baadhi ya familia hazijaweza hata sasa kuwapata ndugu zao waliouawa wakati wa vurugu hizo ili kuwafanyia mazishi kwa utaratibu kijamii na kiibada. Hali hii imeacha jamaa mbalimbali katika simanzi kubwa ya misiba na maombelezo yasiyoelezeka.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), limeguswa na kuumizwa sana na matukio hayo yasiyokuwa ya kawaida. KKKT kama sehemu ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania, na Kanisa la Mungu kwa upana wake linaungana na watu wote wenye mapenzi mema kwa nchi ya Tanzania. Hivyo, KKKT;

1. Limehuzunishwa na kusikitishwa na matukio haya yaliyokosa utu, heshima na thamani ya binadamu. Kanisa linakemea matukio hayo yanayomchukiza Mungu.
2. Kutoa pole kwa jamii na familia zilizopoteza wapendwa wake kwa kuuawa au bado hawajapatikana bila maelezo ya kuridhisha.
3. Kutoa pole kwa uharibifu wa mali za umma na za Binafsi uliofanyika.
4. Kuwaombea wafiwa wote, majeruhi, watu ambao bado hawajapatikana na wanaoshikiliwa bila hatia.
5. Kuomba Toba na rehema kwa Mungu ili nchi yetu iliyoshuhudia umwagaji wa damu za watu ipate kuokolewa dhidi ya ghadhabu ya Mungu juu ya chukizo hili na ipate neema ya kurejea katika Amani.
   Waebrania 4:16 Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

## Wito kwa washarika wote wa KKKT

1. Kanisa linatambua kuwa kila mahali katika makanisa yetu, maombi yamekuwa yakifanyika kuombea amani ya nchi yetu na kuombea uchaguzi mkuu pia. Kanisa linawashukuru waumini wake wote kwa kutekeleza wajibu huo.
2. Kanisa linatoa wito kwa washarika wake wote kuwa na maombi maalum kwa wiki nzima kuanzia ibada zote za Jumapili ya tarehe 16 Novemba 2025. Kisha kila siku maombi yaendelee hadi Jumapili ya tarehe 23 Novemba 2025. Kwa siku za Jumapili, ujumbe wa Kalenda utumike ila katikati ya wiki utaratibu ufuatao unaweza kutumika.

Evangelical Lutheran Church in Tanzania (ELCT)
Boma Rd, Plot #66, P O Box 3033, Arusha, Tanzania
Website: www. elct.or.tz | Email: elcthq@elct.or.tz
Tel: +255 27 250 8856/7 | Fax: +255 27 254 8858 | SG. Direct line: +255 27 250 2511

a. **Jumatatu – Kuwaombea familia zilizopoteza wapendwa wao.**
Maombi ya siku hii yaongozwe na wanawake.

- *"BWANA yu karibu nao waliovunjika moyo, na waliopondeka roho huwaokoa."* — **Zaburi 34:18**

b. **Jumanne – Kuwaombea majeruhi wote.**
Maombi ya siku hii yaongozwe na vijana.

- *"Maana nitakurudishia afya,nami nitakuponya jeraha zako, asema BWANA…*— **Yeremia 30:17a**

c. **Jumatano – Kuomba kwa ajili ya viongozi na mamlaka za Serikali, Mungu awape hekima na moyo wa toba.**
Maombi ya siku hii yaongozwe na wanaume.

- *"Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote. Kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi Maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu"* — **1 Timotheo 2:1–2**

d**. Alhamisi – Kuombea amani ya nchi hasa vyombo vya ulinzi na usalama.**
Maombi ya siku hii yaongozwe na vikundi vya kwaya.

- *"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao. Na amani ikae ndani ya kuta zako, kufanikiwa ndani ya majumba yako."* — **Zaburi 122:6-7**

e**. Ijumaa – Kuombea Kanisa na vyombo vyake.**
Maombi ya siku hii yaongozwe na vikundi vya *fellowship*.

- *"Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo."* — **1 Wakorintho 12:12**

f. **Jumamosi – Kuombea vyombo vya utoaji haki katika nchi hasa mahakama.**
Maombi ya siku hii yaongozwe na vikundi vya Jumuiya.

- *"Bwana wa majeshi amesema hivi, ya kwamba, Fanyeni hukumu za kweli, kila mtu na amwonee ndugu yake rehema na huruma."* — **Zekaria 7:9**

- *"Haki na hukumu ndio msingi wa kiti chako. Fadhili na kweli zahudhuria mbele za uso wako."* — **Zaburi 89:14**

**g. Jumapili ya mwisho (23 Novemba) – Siku ya kumshukuru Mungu.**

- *"Mshukuruni BWANA kwa kuwa ni mwema, kwa maana fadhili zake ni za milele."* **— Zaburi 107:1**

3. Wanataaluma wote wa Huduma ya Ushauri Kichungaji (*Clinical Pastoral Education*) katika Dayosisi zote za KKKT watumie muda huu kutoa tiba ya nafsi na roho kwa wote walioumizwa.

Evangelical Lutheran Church in Tanzania (ELCT)
Boma Rd, Plot #66, P O Box 3033, Arusha, Tanzania
Website: www. elct.or.tz | Email: elcthq@elct.or.tz
Tel: +255 27 250 8856/7 | Fax: +255 27 254 8858 | SG. Direct line: +255 27 250 2511

**Wito kwa Serikali na vyombo vyake**

1. Kanisa linatoa wito kwa Serikali kusikiliza na kushughulikia malalamiko ya wananchi kwa namna ya kujenga umoja wa kitaifa na utengamano wa kijamii.
2. Kanisa linatoa wito kwa Serikali kuwatendea haki raia wote waliopoteza maisha au walioathiriwa.
3. Kanisa linakumbusha kuwa matumizi ya nguvu ya kupita kiasi kwa yeyote hayawezi kuleta baraka na Neno la Mungu linaonya kuwa "Hasira ya Mwanadamu haiitendi haki ya Mungu." (Yakobo 1:20) tena "Wenye haki wakiwa na amri, watu hufurahi; (Mithali 29:2a ).

Mungu ibariki Tanzania.

KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA
EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA
P. O. Box 3033
ARUSHA-TANZANIA

**Imetolewa na Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa**
**Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT)**